JARIDA MTANDAO LA

# UBUNGO MANISPAA

TOLEO NO 3

www.ubungomc.go.tz /Kitengo cha Mawasiliano Serikalini /Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo



## "UBUNGO YETU, FAHARI YETU"



Haliuzwi

# TAHARIRI
## Miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika

Kongole kwa Mheshimiwa Rais wa awamu ya sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wa kutaka maadhimisho ya miaka 61 ya uhuru wa Tanzania Bara yaazimishwe kwa kufanya midahalo na makongamano kwa ajili ya kupata fursa ya kujadili, kuchangia na kupata ufafanuzi wa maendeleo endelevu yaliyofikiwa katika kipindi cha miaka 61 ya uhuru wa Nchi yetu na kufanya shughuli mbalimbali za kijamii huku fedha za maadhimisho hayo zikilekezwe kujenga mabweni kwenye shule zenye watoto wenye mahitaji maalum.

Tarehe 9 Disemba ni siku ambayo Nchi yetu imekuwa ikiazimisha siku ya Uhuru wake ambayo imekuwa ikiazimishwa kila mwaka lengo ikiwa ni kuendelea kuienzi, kujali na kuthamini juhudi kubwa zilizofanywa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere za kupigania uhuru wa Nchi yetu.

Katika siku hiyo ya tarehe 9 Desemba, 1961 mambo makubwa mawili yalifanyika ikiwa kama ni sehemu ya maadhimisho ya siku hiyo ikiwemo kushusha bendera ya mkoloni na kupandisha bendera ya Taifa na kupandisha mwenge wa uhuru kwenye kilele cha mlima Kilimanjaro.

Kushushwa kwa bendera ya mkoloni na kupandishwa kwa bendera ya taifa letu lilikuwa ni tukio kubwa sana kwa watanganyika kwa wakati huo kwani lilikuwa ni ishara ya kuondoka kwa mkoloni na kwamba kuanzia wakati huo Watanganyika watakuwa huru kufanya mambo yao wenyewe kwa mustakabali wao.

Wakati wa upandishaji wa mwenge wa uhuru kwenye kilele cha mlima Kilimanjaro baba wa taifa mwalimu Julius Nyerere alisema “Tunataka kuwasha Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka yetu; ulete tumaini pale ambapo hakuna matumaini; upendo mahali palipo na chuki na heshima palipojaa dharau”.

Maazimisho ya miaka 61 ya uhuru wa Nchi yetu kwa mwaka huu wa 2022 kwa namna yalivyoazimishwa yamekuwa ni chachu kwa kila mmoja wetu kuanzia kwa wananchi, wazee, viongozi wa kisiasa na kidini, taasisi za umma, watumishi na wadau mbalimbali wa maendeleo kuendelea kujitathimini kwa kujipima juu ya mafanikio ambayo nchi imeyafikia kiuchumi, kisiasa na kijamii kwani kila mmoja anajukumu la kufanya ili kuyafikia maendeleo ya Nchi yetu.

Kabla ya ujio wa wakoloni Nchini na walipokuja waingereza walipendekeza majina yao ambayo pia wazee wa kipindi hicho walikataa nchi kupewa majina tofauti na ya asili yetu na mwishowe nchi hii iliitwa Tanganyika, na mwishowe wanaharakati wa kipindi hicho akiwemo hayati mwl. Julius Kambarage Nyerere na wenzie walianza kupigania uhuru wa nchi hii na baada ya uhuru kupatikana ndipo Tanganyika ikaungana na Nchi ya Zanzibar na kupatikana kwa nchi moja iitwayo Tanzania ambapo muunganao ulifanyika mnamo 1964.

Miaka 61 ya uhuru wa Tanganyika, ambapo kwa sasa inajulikana kwa jina la Tanzania kutokana na muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, ni wakati wa kila mmoja kujitathmini na kupima je Nchi yetu imefanikiwa kufika mahali ambapo waliopigania uhuru wakati ule walitaka tufike, maendeleo hayana chama, dini wala kabila kila mmoja ana jukumu la kufanya ili kuyafikia maendeleo ya Nchi yetu.




# UBUNGO MANISPAA YAAZIMISHA YA MIAKA 61 YA UHURU WA TANGANYIKA, 9 DISEMBA

Na Mwandishi Wetu

Tarehe 9 Disemba ni tarehe ambayo Nchi yetu imekuwa ikiazimisha siku ya Uhuru wake ambayo imekuwa ikiazimishwa kila mwaka lengo ikiwa ni kuendelea kuienzi, kujali na kuthamini juhudi kubwa zilizofanywa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere za kupigania uhuru wa Nchi yetu.

Kwa umuhimu huo leo tarehe 09 Disemba, 2022 Manispaa ya Ubungo imeazimisha siku hiyo iliyoenda sambamba na kauli mbiu isemayo “Amani na umoja ni nguzo ya maendeleo yetu” kwa kufanya mdahalo wa kujadili mada mbalimbali juu ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yaliyofikiwa tangu uhuru hadi sasa.

Kongamano hilo liliofanyika siku ya kilele cha maazimisho hayo katika ukumbi wa chuo kikuu cha Dar es salaam lilijumuisha wananchi, wazee, viongozi wa kisiasa na kidini, taasisi za umma, watumishi na wadau mbalimbali wa maendeleo wa Manispaa hiyo lengo ikiwa kupata fursa ya kila mmoja kujadili, kuchangia na kupata ufafanuzi wa maendeleo endelevu yaliyofikiwa katika kipindi cha miaka 61 ya uhuru wa Nchi yetu.

Maazimisho ya sherehe hizo ni tofauti na ilivyokuwa ikiazimishwa kwa miaka ya nyuma ambapo mwaka huu maazimisho hayo yamefanyika kwa kufanya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo wananchi kufanya usafi, michezo, kupanda miti na kuendesha mdahalo kama ambavyo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa awamu ya sita alivyoeleza fedha zilizokuwa zikitumika kwa ajili ya maazimisho hayo zielekezwe kujenga mabweni kwenye shule zenye watoto wenye mahitaji maalum.

Akiongea wakati wa kufungua kongamano hilo Mhe. Kheri James Mkuu wa Wilaya ya Ubungo ameeleza kwa kipindi cha miaka 61 ya uhuru Tanzania imeweza kufikia maendeleo kwa nyanja mbalimbali ikiwemo elimu bure kuanzia darasa la awali hadi kidato cha sita, mpango wa kuhakikisha kila mwananchi anapata uhakika wa matibabu kwa kuwa na bima, ukopeshaji wa mikopo 10% isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Inaendelea Ukurasa wa 2........



Na Mwandishi Wetu

James alifafanua kuwa, Uboreshaji wa miundombinu ya elimu, afya, masoko na barabara imeendelea kuonesha maendeleo yaliyofikiwa na Nchi ambayo ndio yanatafsiri kwa vitendo maana ya maendeleo kwa wananchi wake

Kisiasa, idadi ya viongozi wanawake kuanzia ngazi za chini hadi nafasi za juu za uongozi nchini zimendelea kuongezeka lengo ikiwa ni kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika kuchangia maendeleo.

"Kuazimisha maazimisho hayo kwa njia ya mdahalo ni kupata nafasi ya kutoa elimu zaidi ya kurithisha ujuzi, historia na maarifa ya tulipotoka, tulipo na tunapokwenda kwa kizazi na kwa makundi ya kijamii ili kujenga uelewa wa historia ya Nchi yetu" alisema Mhe. James.

Aidha, James alisema kuwa tuna poenzi miaka 61 ya uhuru ni muhimu kila mmoja kujitathimini kwenye mafanikio tuliyoyafikia kiuchumi, kisiasa na kijamii kwani kila mtu kwa nafasi yake anawajibu wa kuhakikisha anachangia maendeleo ya nchi.

"Kama ambavyo Mwalimu Julius Nyerere alivyoweza kuonesha uzalendo wa kupigania uhuru wa nchi yetu kila mmoja ahakikishe analinda amani, umoja na maendeleo kwani ndio utanzania wetu bila kujali dini, makabila na jinsia" alisema James.

katika kuadhimisha miaka 61 ya uhuru, Manispaa ya ubungo imependelewa kwa kuwa na miradi mingi mikubwa ikiwemo mradi wa ujenzi wa barabara ya njia nane ya kutoka kimara hadi kibaha, kituo kikuu cha kisasa cha Mabasi yaendayo mikoani na Nchi jirani "Magufuli Bus Terminal" mradi mkubwa wa maji wa DAWASA, na uwepo wa vyuo vingi vya mfano ikiwemo chuo kikuu cha Dar es salaam "UDSM" Chuo cha usafirishaji Tanzania "NIT" chuo cha sheria "Law School" na kuwepo kwa mall kubwa ya "Mlimani city mall" na mengine mengi mazuri.

Katika majadiliano hayo washiriki walifanikiwa kupata Mada mbalimbali juu ya masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ambazo zilitolewa na wataalamu mbalimbali akiwemo Prof. Kitila Mkumbo mbunge wa jimbo la Ubungo, Dr. Victoria Lihiru na Dr. Richard Mbunda ambao ni wahadhiri wa chuo kikuu cha Dar es Salaam ambao walitoa mada mbalimbali juu ya masuala ya maendeleo tuliyoyafikia.



# RC MAKALLA AIPONGEZA UBUNGO KWA UJENZI VYUMBA VYA MADARASA

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla ameipongeza Manispaa ya Ubungo kwa juhudi za ukamilishaji wa mradi wa ujenzi wa vyumba madarasa 81 ikiwa ni maandalizi ya kuwapokea wanafunzi 15,008 wakiwemo wasichana 7,632 na wavulana 7,376 wa kidato cha kwanza kwa mwaka 2023.

Amezitoa Pongezi hizo wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa mradi wa madarasa katika Manispaa hiyo lengo ikiwa ni kuhakikisha miradi hiyo inatekelezeka kwa ufanisi na kukamilika kwa wakati ambapo ameridhishwa na kasi na kiwango cha ubora katika utekelezaji wa mradi huo

Makalla alieleza kuwa, Mkoa wa Dar es Salaam umepokea shilingi Bilioni 12.3 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 618 mkoani humo ambapo Manispaa ya - Ubungo ilipokea shilingi Bilioni 1.62 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 81 vya madarasa kwenye shule 10 za Sekondari za Manispaa hiyo.

“Hakika bila kupepesa macho Ubungo mmefanya vizuri kwenye utekelezaji wa mradi huu, na ni dhahili madarasa haya yatakamilika kwa wakati kama mlivyofanya kwenye madarasa ya Uviko” Alisema Mhe. Makalla.

Pamoja na pongezi hizo , Makalla alimtaka Beatrice Dominic Mkurugenzi wa Manispaa Ubungo kuhakikisha maeneo yote ya shule yanapimwa na kuwa na hati miliki ya ardhi pamoja na kuwekewa uzio ili kukabailiana na changamoto ya uvamizi wa maeneo hayo. Aidha wananchi wametakiwa kulinda miundombinu yote ya shule ili shule hizo zibaki katika ubora wake na kutumika kwa muda mrefu.

“Wananchi na Wenyeviti wa Mitaa lindeni mipaka ya Shule zilizopo kwenye maeneo yenu ili kuepuka uvamizi wa maeneo ya Shule hizo” alisisitiza Makalla.

Kwa upande wake Beatrice Dominic Mkurugenzi wa Manispaa hiyo amesema katika utekelezaji wa mradi wa madarasa hayo madarasa 27 yameshakamilika na madarasa 54 yako kwenye hatua ya ukamirishaji ambapo hadi kufikia tarehe 25 Disemba, 2022 madarasa yote yatakuwa yamekamirika yakiwa na viti na meza za wanafunzi.

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ilipokea kiasi cha shilingi Bilioni 2.62 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 katika shule 10 zilizokuwa na upungufu wa madarasa kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2023.

Kwa mwaka 2023 Manispaa ya Ubungo inatarajia kupokea idadi ya wanafunzi 15,008 wakiwemo wasichana 7,632 na wavulana 7,376 wa kidato cha kwanza ambao watakuwa na uhakika wa kusoma wakiwa madarasani kwani Rais wa awamu ya sita Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuboresha vya kutosha miundombinu ya elimu kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania.



# NAIBU WAZIRI NDEJEMBI ATEMBELEA UBUNGO

Na Mwandishi Wetu.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi (MB) amesema Serikali ya awamu ya sita ya Tanzania inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya miezi 20 ya uongozi wake imeendelea kusimamia stahiki za watumishi ikiwemo upandaji wa madaraja, kulipwa kwa malimbikizo ya mishahara na mengine mengi mazuri ya kiutumishi.

Hayo ameyasema leo akiwa kwenye ziara yake ya kuitembelea Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo wakati anasikiliza changamoto za watumishi wa manispaa hiyo ambapo pia alifanya ukaguzi wa kikundi cha wanufaika wa TASAF wilayani humo.

Ndejembi amewataka watumishi wa Manispaa hiyo kuhakikisha wanampango kazi wa kutekeleza majukumu yao ya kila siku ikiwa ni pamoja na kuwa wabunifu, kuwajibika ipasavyo na kutoa huduma bora ili kuendelea kutatua kero za wananchi kwa maslahi ya Taifa kwa ujumla.

Aidha, Ndejembi amewataka watumishi hao kuacha kufanya kazi kwa mazoea na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa hiyo Ndg. Beatrice Dominic ameeleza kuwa Manispaa ya Ubungo ina idadi ya watumishi 4,397, watumishi 218 walibadilishiwa Muundo kutokana na kujiendeleza kielimu, 742 - wamepanda madaraja kwa mujibu wa kanuni za kiutumishi na watumishi 1,559 malimbikizo yao yalilipwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na stahiki zingine za watumishi zinaendelea kutolewa.

Nae Mkuu wa Wilaya hiyo Mhe. Kheri James amesema Manispaa ya Ubungo inajivunia kwa mapinduzi makubwa yanayofanywa na Serikali katika kuleta mageuzi ya haki na kuzingatia stahiki za watumishi.

“Tunaona mageuzi makubwa yanayofanywa kwenye upandishwaji wa vyeo kwa watumishi, mafao ya watumishi, ongezeko la mishahara ya watumishi na mengine mengi mazuri yanayofanywa na Serikali ya awamu ya sita” Alisema James.



# RHMT MKOA WA DAR ES SALAAM YATEMBELEA UBUNGO

Na Mwandishi Wetu

Timu ya uendeshaji wa huduma za afya Mkoa wa Dar es Salaam "RHMT" imefanya ziara ya usimamizi shirikishi Manispaa ya Ubungo na kutembelea kituo cha afya cha Sinza na Mbezi kwa ajili ya kuangalia utoaji wa huduma za afya katika vituo hivyo ikiwemo huduma ya lishe, dawa, huduma ya baba, mama na mtoto na uwepo wa vifaa na vifaa tiba.

Ziara hiyo imefanyika leo tarehe 21 Disemba, 2022 ambapo timu hiyo ikiongozwa na Mganga Mkuu wa Mkoa Dkt. Rashid Mfaume imeipongeza Manispaa ya Ubungo kwa kuendelea kusimamia vizuri utoaji wa huduma - za afya kwa usimamizi bora wa miradi, kuongeza vifaa tiba, uwepo wa dawa na vitendea kazi vyote kulingana na ngazi ya kituo cha kutolea huduma za afya.


Akiongea Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Dkt. Mfaume amepongeza hatua za matayarisho ya kuanza kutoa huduma kwenye vituo viwili vipya ikiwemo kituo cha afya Goba na Zahanati ya Kinzudi ifikapo mwezi Januari, 2023 ambavyo vitasaidia kusogeza huduma za afya ka ribu na wananchi.

Kwa upande wa Mganga Mkuu wa Manispaa ya Ubungo Dkt. Peter Nsanya ameahidi kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya ndani ya Manispaa hiyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vituo vipya vinaanza kutoa huduma ifikapo januari, 2023, kusimamia miradi, kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na utoaji wa elimu ya masuala mbalimbali ya afya.

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina jumla ya vituo 22 vya kutolea huduma za afya ikiwemo Hospitali 1, vituo vya afya 5 na Zahanati 16 ambavyo vinaendelea kutoa huduma za afya kwa wananchi.



*Muonekano wa moja kati ya majengo ya madarasa 81 kwa shule 10 za Sekondari za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo zilizojengwa na Fedha kutoka Serikali kuu za kapu la mama (Mheshimiwa Rais wa awamu ya sita Dkt. Samia Suluhu Hassan) kwa ajili ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023. #ubungoyetu,fahariyetu #kaziiendelee*







# MADIWANI UBUNGO WAPEWA SEMINA KUHUSU MFUMO WA USAJILI WA VIKUNDI

Na mwandishi Wetu

Madiwani wa Manispaa ya ubungo wametakiwa kuwa chachu ya kuhamasisha wananchi katika maeneo yao kusajili vikundi vya wananwake , vijana na watu wenye ulemavu kupitia mfumo mpya wa usajili wa vikundi na usimamizi wa mikopo ya 10% inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ili waweze kupata mikopo hiyo.

Madiwani hao walielezwa jukumu hilo na Rose Mpeleta Afisa Maendeleo ya jamii wa Manispaa hiyo kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo madiwani juu ya uwepo wa mfumo huo mpya na kusema kuwa kikundi ambacho hakitajisajili kwenye mfumo huo hakitapata Mkopo kwani maombi ya mkopo yanawasilishwa kwenye mfumo.

Mpeleta alisema kuwa mfumo huo ni mpya na umeandaliwa na wizara ya Ofisi ya Rais TAMISEMI lengo ikiwa ni kutatua changamoto mbalimbali za mikopo hiyo ikiwemo marejesho, hivyo Wanakikundi wanatakiwa kutembelea kiunganishi cha mikopohalmashauri.go.tz ili kusajili vikundi vyao katika mfumo huo.

Nae Afisa TEHAMA anayehusika na usimamizi wa mfumo huo kwa Manispaa ya Ubungo Ndg Aziza Lotta amesema kuwa mfumo huo utasaidia kusajili vikundi katika namna bora zaidi na pia utarahisisha ufuatiliaji wa marejesho kwa vikundi vitakavyopatiwa mkopo kwani marejesho yao sasa watakua wanayafanya kwa kutumia namba za kumbukumbu (control number) watakazopewa na ofisi ya Maendeleo ya jamii tofauti na awali.

Kwa upande wake diwani wa goba Mhe. Ester Ndoha aliipongeza Manispaa kwa kuendesha mafunzo hayo kwani yamewasaidia kuelewa mfumo huo ambao utawasaidia wananchi kutumia fursa ya kupata mikopo isiyo na riba kwa ajili kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Inaendelea Ukurasa wa 8........




***Kikundi cha vijana cha bajaji kilichonufaika na mikopo 10% ya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri***

"Sisi kama viongozi na wawakilishi wa wananchi tutahamasisha wananchi kujisajili kwenye mfumo huu ili waweze kupata mikopo ambayo inatokana na kodi zao kama sheria inavyoelekeza" alisema Mhe. Ester

Mpaka sasa vikundi ambavyo vilivyojisajili kwenye mfumo ni 286 ambapo vyeti 211 vimeshatolewa kwa vikundi husika.

Aidha kwa vikundi ambavyo bado havijajisajili kwenye mfumo vinatakiwa kufika kwenye ofisi za kata na kuonana na afisa maendeleo wa kata ambaye atawasaidia kwenye zoezi zima la usajili, pia watembelee ukurasa wa Youtube wa UBUNGO MANISPAA kisha watafute "Jinsi ya kusajili kikundi kwenye Mfumo" hapo watapata video yenye maelezo yote kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa hatua za usajili.



# UJENZI WA OFISI YA UDHIBITI UBORA WA SHULE UBUNGO MC WAANZA.

Na Mwandishi Wetu

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James aliipongeza Kamati inayosimamia ujenzi wa ofisi ya Mdhibiti ubora wa Manispaa ya Ubungo inayojengwa Kata ya Kwembe wilayani hapo na aliwataka kuzingatia ubora ili kulinda dhamira ya dhati ya Mhe. Rais wa awamu ya sita ya kuhakikisha elimu bora inatolewa kwa shule zote za msingi na sekondari.

Pongezi hizo alizitoa wakati wa ziara aliyoifanya ya kutembelea utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ofisi hiyo kwa lengo la kuona - ubora na ufanisi wa utekelezaji wa mradi huo.

Sambamba na pongezi hizo Mhe. James alisema ujenzi wa Ofisi hiyo utaenda kuongeza ufanisi, uadilifu na tija ya utoaji elimu kwa shule za msingi na sekondari kwani ofisi ya udhibiti ubora inajukumu la kusimamia na kudhibiti ubora wa elimu unaotolewa shuleni.

Kwa upande wake, Mdhibiti Ubora wa Manispaa ya Ubungo Bi. Marrietha Mkai alisema Manispaa ya Ubungo imepokea kiasi cha shilingi Milioni 181 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambao utakamilika mnamo tarehe 30 Disemba, 2022.

Aidha, Bi. Marietha alisema Manispaa ya Ubungo ilipokea mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo kutoka kwa mdau anaemiliki shule ya Greenbelt.

Kwa sasa ofisi za udhibiti ubora wa shule zipo ndani ya jengo la ofisi ya Manispaa ya Ubungo.



*Ziara ya kikazi ya Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi (MB) wa pili kushuto kwenye picha ya juu na wa kwanza kushoto kwenye picha ya chini alipotembelea Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ambapo akiwa katika Manispaa hiyo alikagua kikundi cha wanufaika wa TASAF na aliongea na watumishi wa Manispaa hiyo*





# WATU LAKI MBILI WANATUMIA MWENDOKASI KWA SIKU, DART

Na Mwandishi Wetu

Wakala wa usafiri Dar es Salaam (DART) inatarajia kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kupitia mabasi ya mwendo kasi kwa kuongeza idadi ya mabasi ya usafiri ili kutatua changamoto ya msongamano wa abiria kwenye mabasi pamoja na abiria kusubiri kwa muda mrefu vituoni.

Kauli hii imetolewa na Mkurugenzi wa DART Dr. Edwin Mhende wakati wa kikao kilicholenga kutoa elimu ya matumizi sahihi ya miundombinu ya usafiri kwa watumiaji wa vyombo vya moto kilichohudhuliwa na wakuu wa wilaya za Ubungo, Kinondoni, Kigamboni na Kibaha pamoja na watalamu.
Akiwaeleza watumiaji wa miundombinu hiyo Dr. Mhende alieleza kuwa madhumuni ya kutoa elimu hiyo nimkakati wa kuhakikisha miundombinu hiyo inatunzwa na kutumiwa kwa matumizi lengwa yaliyoainishwa na DART.

Pamoja na kutoa elimu kwa watumiaji wa vyombo vya moto Dr. Mhede alieleza kuwa kwa sasa usafiri wa mwendokasi katika jiji la Dar Es Salaam unazidi kushika kasi kila siku kutokana na ongezeko la watumiaji ambapo kwasasa takwimu zinaonesha kuwa UDART wanasafirisha watu 180,000 – 200,000 kupitia mabasi 210 yaliyopo kwa sasa kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri wa Umma kwa maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam.

Hivyo basi, Dr. Mhede ameeleza kuwa DART inatarajia kusaini mkataba na mtoa huduma mwingine atakaeongeza mabasi mengine 177kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma hiyo

Kwa upande wa mgeni rasmi katika kikao hicho mkuu wa wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James ameipongeza DART kwa kufanya kazi nzuri ya kusimamia usafiri wa mwendokasi na amewataka kuendelea kujitahidi kumaliza changamoto zilizopo ili kuleta ufanisi wa huduma.

“Pamoja na kazi kubwa mnayofanya lakini uhitaji kwa wananchi bado ni mkubwa hivyo mnatakiwa kupanua wigo wa utoaji huduma hiyo” alisema

Aidha kheri amewaomba vingozi, wananchi na wadau mbalimbali kulinda miundombinu ya mwendokasi ili tija yake idumu kwa muda mrefu



BARAZA LA MADIWANI MANISPAA YA UBUNGO PAMOJA NA WAJUMBE WA CMT WAKIWA NA MKURUGENZI WA MANISPAA YA KAHAMA KATIKA PICHA YA PAMOJA BAADA YA KUPATA MAFUNZO KUHUSU MASWALA YA UKUSANYAJI WA MAPATO WALIPO-TEMBELEA MANISPAA YA KAHAMA




KIKUNDI CHA VIJANA CHA BAJAJI KILICHONUFAIKA NA MIKOPO 10% YA WAJASIRIAMA-LI WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU KWA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI



# WATENDAJI KATA UBUNGO WASAINISHWA MIKATABA YA LISHE

Na Mwandishi Wetu

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Kheri James amewataka watendaji Kata kuweka mikakati ya kuwezesha watoto kupata chakula wakiwa shule kwa kushirikiana na kamati za shule, walimu wakuu na wazazi au walezi ili watoto wawe na afya bora kimwili na kiakili na hivyo kuimarisha ufaulu.

Agizo hilo alilitoa kwenye hafla ya kusaini mikataba ya lishe baina ya Mkurugenzi na Watendaji Kata 14 za Manispaa hiyo, lengo ikiwa ni kuendelea kusimamia mikakati ya Serikali katika kuhakikisha wananchi wake hususani watoto na wajawazito - wanakuwa na lishe bora.

James alisisitiza kuwa, ni jukumu la kila mmoja kuanzia ngazi ya Halmashauri hadi Mtaa kuhakikisha mpango wa lishe unasimamiwa vizuri na kuondoa udumavu, aidha alitoa pongezi kwa Kata zilizotekeleza vizuri mkakati wa lishe na kufanikiwa kupambana na udumavu kutoka 8% hadi kufikia 1.1% kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

“Lishe duni inammadhara mengi ikiwemo Kukwamisha ukuaji wa viungo na ubongo na hivyo kuwa na madhara yasiyorekebishika kielimu, ajira na mustakabali wa maisha yake” Alisema James

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa lishe kwa ngazi ya Halmashauri kwa robo ya kwanza 2022/2023 Ndg. Beatrice Mossile Afisa lishe wa Manispaa hiyo alisema kuwa Kitengo cha lishe kimefanikiwa kutoa elimu kwa Madiwani 19, walimu wakuu wa Shule za msingi na Sekondari, walimu wa day care na walimu wa afya na kutoa matibabu kwa watoto wenye utapiamlo.

Kutokana na mafunzo yaliyotelewa Halmashauri imefanikiwa kuwa na Shule 192 zenye club za afya na lishe ambayo ni Sawa na 74.4% ya shule zote 258, uwepo wa Shule 90 za msingi na Sekond-

Inaendelea Ukurasa wa 14......



ari zinazotumia unga wa mahindi uliowekwa virutubisho na uwepo kwa mashine 7 kati ya 10 zinazohitajika za kusaga lishe ambayo ni sawa na 70%.

Mossile, aliendelea kueleza kuwa Manispaa hiyo kwa sasa imefanikiwa kupambana na tatizo la udumavu kutoka 8% hadi kufikia 1.1% na hivyo matarajio ya Manispaa kwa sasa ni kuhakikisha idara ya elimu msingi na sekondari wanashirikiana vizuri na Kam ati za shule, wazazi au walezi ili kukubaliana namna ya kuwezesha wanafunzi kupata chakula wakiwa shule kama muongozo wa lishe unavyoeleza.





**Picha ya juu ni ya muonekano wa barabara ya kijazi na picha ya chini ni muonekano wa barabara ya njia nane ya kutokea kimara hadi kibaha, Manispaa ya Ubungo inapongeza juhudi Serikali za kuendeleza miundombinu ya barabara ambayo inaenda kupunguza foleni na hivyo kuwezesha wafanya biashara kuwa na mazingira bora ya kuendesha biashara zao na hivyo kukuza uchumi wa Nchi.**



# WAGANGA WAFAWIDHI, TIBA MBADALA UBUNGO WATAKIWA KUZINGATIA TAHADHARI ZA EBOLA

Na Mwandishi Wetu


Kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Ebola uliotokea Nchi jirani ya Uganda Manispaa ya Ubungo imekutana na waganga wafawidhi wa vituo vya Serikali na binafsi pamoja na wataalam wa tiba za asili lengo ikiwa ni kuona utayari kwenye vituo vyao na jamii namna ya kujikinga dhidi ya ugonjwa huo.

Wataalamu hao wameelekezwa namna ya kumtambua mshukiwa wa ugonjwa wa Ebola na wametakiwa kuwa na sehemu maalum ya washukiwa wa ugonjwa huo, kuboresha namna ya kujikinga -na Ebola na wameelezwa namna ya kujikinga na ugonjwa huo.

Akiongea Dkt Felista Kimolo Mratibu wa huduma za dharura na majanga Manispaa ya Ubungo ameeleza kuwa Ebola ni ugonjwa hatari na tayari umeshatokea Nchi jirani ya Uganda hivyo ni vyema kuweka mikakati ya kujikinga dhidi ya Ugonjwa huo hatari.

Nae mganga mkuu wa Manispaa ya Ubungo Dkt Peter Nsanya amewataka wataalamu hao kuhakikisha wanaweka vyumba vya dharura kwa ajili ya washukiwa wa ugonjwa huo.

Aidha, Nsanya amewataka wataalamu hao kutoa huduma kwa weledi na kusimamia mikakati iliyowekwa juu ya udhibiti wa ugonjwa wa ebola.



# ELIMU KUTUMIKA KUKOMESHA UKATILI WA KIJINSIA UBUNGO

Na Mwandishi Wetu

Kamati ya Ulinzi na Usalama wa mtoto Manispaa ya Ubungo imepanga kutoa elimu kwa jamii namna ya kudhibiti na kukomesha matukio ya unyanyasaji kwa wanawake na watoto ili kuwa na jamii yenye haki na usawa.

Kamati imebainisha Mkakati huo kwenye kikao cha kujadili taarifa za utekelezaji wa kamati hiyo kwa kipindi cha robo ya kwanza (julai – septemba 2022) ambapo watoto wameonekana kuwa wahanga wa vitendo vya unyanyasaji hasa wa kingono katika mazingira mbalimbali ikiwemo shule, kweny jamii na majumbani.

Suala la lishe pia ni jambo la msingi katika kuangalia ulinzi na usalama wa mtoto, hivyo kamati imeshauri shule ziwe na somo la mapishi kwa videndo ili watoto waweze kujipikia pale wazazi au walezi wanapokuwa kwenye majukumu mengine.

Ili familia ziwe na uhakika wa chakula hasa kwa wanawake wajane, wanawake wameshauriwa kujishughulisha na biashara ndogondogo ilikuwa na usalama wa chakula katika familia badala ya kuwa ombaomba au kusubiri msaada hali inayopelekea lishe duni hasa kwa watoto na wajawazito.

Akieleza utekelezaji wa shughuli za kamati hiyo Afisa Ustawi wa jamii Manispaa hiyo ndugu Zainabu Masilamba ameeleza kuwa, katika kipindi cha julai hadi septemba 2022 matukio ya ukatili yameonekana kukithiri kwenye kata za Mabibo, Kimara, Ubungo, Saranga, Goba, Makuburi, Mburahati na Makurumla.

Inaendelea Ukurasa wa 18.....



Ili kuimarisha ulinzi na usalama wa wanawake na watoto katika jamii ni vema kuimarisha uchumi wa kaya; mazingira salama ya mwanamke na mtoto; malezi bora, kuimarisha mahusiano katika kaya na kuziwezesha familia juu ya haki na wajibu wa mtoto; utekelezaji na usimamizi wa sheria za mtoto; huduma kwa waathirika wa ukatili na mazingira salama shuleni na stadi za maisha.

Wajibu wa Kamati ya ulinzi na usalama wa mwanamke na mtoto kutekeleza vyema Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza ukatili - dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWA) ambao unalenga kusimamia haki na maendeleo ya mtoto na kuzuia ukatili dhidi ya mwanamke na mtoto na kuhakikisha wanapata haki zao na kutimiza wajibu wao vyema.



# RC MAKALLA AFUNGUA HOTEL YA KISASA KITUO CHA MABASI CHA MAGUFULI

Na Mwandishi Wetu


Katika kuendeleza jitahidi za kuibua vyanzo vipya vya mapato ya ndani ya Halmashauri, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla amezindua rasmi mradi wa Hotel ya "Ubungo Executive Lodge" iliyopo katika kituo kikuu cha Mabasi cha Magufuli.

Akizindua hotel hiyo, RC Makalla ameelekeza hotel kuachwa ijiendeshe kibiashara ili kuleta tija kwa serikali na mwekezaji pia.

Aidha RC Makalla ametaka uendeshaji wa hotel hiyo kuzingatia makubaliano ya kimkataba na uwazi katika kila kitu.

Hoteli hiyo Ina idadi ya vyumba 38 ambavyo vikijaa vyote itaingiza Shilingi Milioni 1.1 kwa siku, Milioni 30 kwa mwezi na Milioni 421 kwa Mwaka ambapo Halmashauri ya Ubungo itachukuwa Asilimia 60 na Mwekezaji Asilimia 40.

Pamoja na hayo RC Makalla ametumia Uzinduzi huo kukemea Wizi na uharibifu wa Vifaa kwenye hotel huku akielekeza Halmashauri ya Ubungo kutafuta Wadau watakaoboresha mandhari ya nje ya Kituo Cha Magufuli ikiwemo Ujenzi wa bustani na sehemu za kupumzika kulingana na hadhi ya Kituo.







WANANCHI NA WAFANYABIASHARA WOTE WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO MNAKUMBUSHWA KUENDELEA KUCHANGIA MAPATO YA MANISPAA KUPITIA VYANZO MBALIMBALI VILIVYOANISHWA

**KODI AU TOZO ZIFUATAZO;**

* USHURU WA HUDUMA

* LESENI ZA BIASHARA

* LESENI ZA VILEO

* VIBALI VYA SHEREHE

* ADA MBALIMBALI

* VIBALI VYA UJENZI

* VIBALI VYA MADINI YA UJENZI

* USHURU WA HOTELI

* USHURU WA KUSHUSHA NA KUPAKIA

**ZINGATIA;**

Kodi yako ina mchango mkubwa sana juu ya maendeleo ya Halmashauri yako.
Ukilipa kodi, miundombinu ya elimu, afya, barabara, maji, na huduma nyingine muhimu zitaboreshwa.
Na hivyo mimi, wewe sote tutapiga hatua.

LIPA KODI, TOZO USHURU NA ADA MBALIMBALI KWA MASLAHI YAKO NA TAIFA KWA UJUMLA KUWA MZALENDO



# TAKUKURU YATOA ELIMU UBUNGO

Na Mwandishi Wetu

TAKUKURU imepewa mamlaka ya kuzuia na kupambana na rushwa kupitia sheria no 11 ya mwaka 2007 na katika kufanikisha hilo Leo tarehe 22/11/2022 ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Ubungo kwa kushirikiana na Manispaa ya Ubungo imetoa semina kwa Madiwani wa manispaa hiyo lengo ikiwa ni kuendelea kuwakumbusha juu ya uwajibikaji unaostahili.

Katika semina hiyo Waheshimiwa Madiwani wamefanikiwa kujifunza mada mbalimbali ikiwemo umuhimu wao juu ya mapambano Mapambano dhidi ya rushwa, maadili ya kiutendaji, majukumu na wajibu wao katika uendeshaji wa shughuli za Halmashauri.

Akiongea katika mafunzo hayo bi Dorothea Mrema Afisa TAKUKURU Mkoa wa kinondoni ameeleza kufanya kazi kwa mazoea, ukosefu wa huduma bora katika jamii, kutosimamia vyema miradi ya maendeleo kunapelekea kuwepo kwa mianya ya rushwa na amewataka viongozi hao kushirikiana vyema na TAKUKURU kwa kutoa taarifa za rushwa, kufuata sheria, kanuni na taratibu ili kuzuia mianya ya rushwa.

Nae Ndg. George Mwendamseke Afisa mwandamizi maadili ya viongozi wa Umma amewataka viongozi hao kusimamia maadili katika uwajibikaji wao ikiwa ni pamoja na kuepuka migongano ya kimaslahi, na hivyo kuwepo kwa ufanyaji kazi na uwajibikaji wa pamoja kwa maslahi ya wananchi.

“Maslahi binafsi yakizidi kuliko maslahi ya Umma Nchi haitaweza kuendelea” alisisitiza Mwendamseke.

Inaendelea Ukurasa wa 22.......





# TAKUKURU WAKITOA ELIMU KWA BARAZA LA MADIWANI MANISPAA YA UBUNGO KUHUSU UKUSANYAJI WA MAPATO

Maximillian Sindagulu Mwakilishi kutoka ofisi ya Mkoa wa Dar es salaam ameeleza wajibu na majukumu ya Madiwani katika uendeshaji wa Halmashauri ikiwa ni pamoja na wajibu wa ukusanyaji wa mapato pamoja na kusimamia shughuli mbalimbali za halmashauri.

Aidha Mhe. Jaffery Nyaigesha Mstahiki Meya wa Manispaa ameipongeza ofisi ya TAKUKURU ya Wilaya hiyo kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yanawezesha Madiwani hao kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na kuahidi kutofanya kazi kinyume na utaratibu, sheria na kanuni zilizowekwa kwa maslahi ya wananchi wa Ubungo.




MADIWANI KUTOKA MANISPAA YA MWANZA JIJI WAKIWA KATIKA STENDI YA MABASI MAGUFULI WALIPOENDA KUJIFUNZA KUHUSU NAMNA BORA YA UKUSANYAJI WA MAPATO



MSTAHIKI MEYA MANISPAA YA UBUNGO JAFFARY NYAIGESHA AKIWA KATIKA PICHA YA PAMOJA NA MADIWANI KUTOKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA



PICHANI NI MADIWANI WA MANISPAA YA UBNGO WAKIWA KATIKA BARAZA



HALIUZWI

OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
LUGURUNI, KWEMBE
UBUNGO, MANISPAA

Jarida hili limehaririwa na kusanifiwa na;
Joina J Nzali

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo

Limeandaliwa na;
Martha J Nicholaus (Afisa Habari)

Barua Pepe: md@ubungomc.go.tz
Tufuatilie kupitia kurasa Ubungo Manispaa / Tovuti www.ubungomc.go.tz